

giza linatoweka katika moyo yetu wakati Yesu anapoingia na kuchukua utawala.

Sijui kama wewe unaweza kuuimba wimbo huu:

Moyoni mwangu, moyoni mwangu
Njoo moyoni, Bwana Yesu!
Njoo naomba, Njoo kwa kukaa!
Njoo moyoni, Bwana Yesu!

Ni dhambi gani ambazo zahitajiwa kusafishwa katika damu ya Yesu? Kutotii, kusema uongo, kudanganya, luiba, kuapa na kutukana, kusema maneno ya uchafu, kuonyesha hasira na mambo mengi mengine ambayo yatuweka chini ya utawala wa Shetani katika ufalme wake wa giza.

Angalia katika picha ya ukurasa wa kwanza na uone jinsi Roho Mtakatifu anavyokaa vizuri katika moyo uliompokea. Unajua ni kwa nini njiwa ni kielelezo cha Roho Mtakatifu? Ni kwa sababu njiwa ni mpole na wala hana hasira na hatia. Roho Mtakatifu ni zaidi ya hayo. Yeye ni Roho ya neema na mamlaka. Anatulinda na kutuwezesha kuishi maishani katika usafi na ushindi.

Je, unapenda sasa hivi kuufungua moyo wako kwa Yesu, ili kwamba Roho wake Mtakatifu aingie kwako? Piga magoti na umwambie hivyo. Unaweza kuomba hivi:

“Yesu, mpenzi, unisamehe kwa kuwa mimi nimekuwa mbaya. Tafadhali ingia

katika moyo wangu. Safisha moyo wangu na damu yako kutoka dhambi zote, hata Shetani asiweze kujificha moyoni mwangu.”

Ujue kwa hakika kabisa kwamba Rafiki yako, Yesu Kristo amekwisha kusikia sala yako hii. Naye amekwisha kukusameche, ikiwa umeomba katika roho ya kweli. Kwa hiyo uwe na furaha na umsifu Yesu, sema AHSANTE kwake juu ya wokovu!

Sasa tia jina lako, anwani na tarehe hapa chini katika karatasi hii, na kumbuka siku hii ambayo ni siku yako ya kumpokea Yesu, Mwokozi wako.

Ukipenda kujua mahali pa kujifunza maneno ya Mungu ama mahali pa shule la Jumapili, au kanisa lililo karibu andika kwetu kwa anwani ya hapa chini. Tutajaribu kukusaidia. Tunawaomba ninyi vijana wote mnaosoma karatasi hii.


Jina langu: _____

Anwani: _____

Tuma kwa: TRACTCENTRE
P.O. Box 48454
NAIROBI, KENYA

au kwa:


Habari njema
kwa watoto!



Kila mvulana na msichana ambaye ana umri wa kutosha ameelewa pia mambo fulani juu ya hali yake. Wameona kuwa wana moyo mbaya. Wame jua kuwa mara nyingi ni rahisi kutenda mabaya kuliko kutenda mema. Inaonekana kwamba mambo ambayo wamekatazwa wasiyafanye, ndiyo yale yale wanafanya. Na mara nyingi huwa wenye kutotii. Na Mungu amesema kuwa kutotii ni dhambi. Dhambi yatupeleka na kutuweka chini ya mamlaka ya Shetani. Tunasoma katika Biblia kuwa Shetani ni “Mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi katika wana wa uasi.” Efe. 2:2.

Ufalme wa Shetani ni ufalme wa giza, na ufalme wa Mungu ndio ufalme wa mwanga. Hiyo ndiyo maana wakati ule tunapofanya mabaya mioyo yetu huhuzunika, lakini tunapofanya mazuri mioyo yetu huwa miepesi na kufurahi. Kila dhambi inafanya moyo kuwa mweusi mpaka kama wasichana na wavulana wamekwisha kua na kuwa vijana mioyo yao ni michafu kabisa. Mungu amesema, “Roho inayotenda dhambi itakufa milele.” Maana yake ni kwamba wenye dhambi wataadhibiwa milele.

Sasa angalia picha ya moyo mweusi! Unaona nini? Nyoka. Unajua kabisa kwamba nyoka hujificha mahali pa giza tena hujaribu asionekane. Ingawa Shetani anajaribu kutushawishi kutenda dhambi, hataki tumwone na kumtambua.



Wakati mavazi yetu yanapokuwa machafu, mama anayafua kwa sabuni na maji.

Lakini ni kitu gani ambacho chaweza kusafisha moyo mweusi wenye dhambi na kuufanya kuwa mweupe na safi?

Lakini sikia habari njema! Mungu aliwapenda wavulana na wasichana na watu wote wa dunia hata alimtoa Mwana wake pekee ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yn. 3:16.

Ilikuwa ni siku kuu ya ajabu kwa wenye dhambi, Mungu alipomtuma Yesu Kristo ili afe badala yetu na kutulipia adhabu yetu ya milele, ili



tuwe huru kutoka dhambi na adhabu na tupate uzima, uzima wa milele.

Kamwe hatuwezi kuiosha moyo michafu kwa sabuni na maji, lakini wakati tunapomwamini Yesu tukiungama dhambi na kumpokea kama Mwokozi wetu, Mungu anasema, “Damu ya Yesu Kristo inasafisha dhambi zote... Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atuondolee dhambi na kutusafisha kabisa.”

Njiwa ni kielelezo cha Roho Mtakatifu. Angalia ni kitu gani kinachotendeka wakati Roho wa Mungu anapoingia kwa kukaa. Ona jinsi nyoka anavyokimbia kwa sababu hawezi kukaa kwenye nuru na kuonekana. Vile vile